




AINAZAMAFUNDO (TYPES OF KNOTS)

BIGHT

Mafundo mengi huanza kufungwa na hatua hii. Hufungwa kwa kuwekwa kulia juu ya kushoto

N.B: Itatumika mara nyingi, iweke kichwani.


Overhand Knot

Hatua:

1. Chukua Kamba iliyo kulia iweke juu ya kushoto.
2. Chukua Kamba iliyopita juu ya mwenzie ili ipite ndani ya tundu lililo wazi.
3. Kaza fundo lako.

Matumizi:

- i. Kuzuia Kamba isianze kuchakaa mwishoni.
- ii. Hukusaidia kupanda juu kwa kutumia Kamba pasipo kutereza.




Fundo la umbo 8 (Figure eight Knot)

Hatua:

1. Shika Kamba yako karibu na mwishoni.
2. Weka kulia juu ya kushoto.
3. Kisha kushoto juu ya kulia.
4. Ie Kamba iliyopita chini ivute kupitia juu kisha pitisha kwenye bite ya kwanza.

Matumizi:

- Kuzuia Kamba isianze kuchakaa.
- Kukazia vifurushi.




Square Knot (Reef Knot)

Hatua:

1. Shika mwisho wa Kamba huku na huku.
2. Weka kulia juu ya kushoto kisha tengeneza over hand.
3. Ila Kamba iliyopita juu, ivute kuingia ndani ya bight.
4. Weka kushoto juu ya kulia.
5. Ila Kamba iliyopita juu, ivute kuingia ndani ya bight.
6. Kisha kaza fundo lako.

Matumizi:

- Kutengeneza vifundo.
- Kufungia vitu mbalimbali kama vifurushi, kuni n-k.
- Hutumika katika huduma ya kwanza.




Sheepshank (Dog Shank)

Hatua:

1. Funga over hand.
2. Igawanye mwisho mmoja kulia mwingine kushoto.
3. Funga mwisho wa kulia na kushoto.

Matumizi:

- Kufupisha kamba
- Huzuia Kamba isitereze.




Two Half Hitches

Hatua:

1. Zungusha Kamba kwenye kitu kifungwacho.
2. Funga clove hitch katika Kamba iliyobaki.

matumizi

- Kutengeneza mahali pa kutundika nguo, mabegi, n-k.
- Kufunga Kamba kwenye mti au nguzo.
- Kuunganisha Kamba 2 zisizofanana (ukitumia fundo hili zitakuwa imara zaidi).




Bow line knot

Hatua:

1. Tengeneza bight karibu na mwishoni mwa Kamba.
2. Chukua mwisho wa kamba kisha pitisha kwenye bight kupitia upande wa chini.
3. Zunguka kamba iliyosimama wima.
4. Rudi kwa njia uliyoingilia.

Matumizi:

- Kufungia wanyama pasipo kuwakaba.
- Kumwoko mtu anayezama maji.




Sheet band knot

Hatua:

1. Tengeneza bight karibu na mwishoni mwa Kamba iliyo nene.
2. Chukua kamba nyembamba kisha ipitisha kwenye bight ya kamba nene.
3. Zunguka kamba ile nene.
4. Kaza kwa kupita chini ya kamba nyembamba.

Matumizi:

- Kufungia bendera.
- Zaweza pia kuunganisha kamba zisizofanana unene.




Timber hitch

Hatua:

1. Tengeneza half hitch.
2. Izungushe kamba kwenye bight iliyozunguka gogo.

Matumizi:

- Kufungia magogo yanayotakiwa kuvutwa.
- Kuanzia kufunga diagonal lashing.



Clove hitch


Hatua:

1. Weka kamba juu ya gogo.
2. Izungushe kamba kwenye gogo huku ukielekea kulia.
3. Ukiika pale kamba ilipoanzia kuzunguka, pita juu ya kamba iliyoanza kisha zunguka kuelekea kushoto.
4. Maliza fundo lako kwa kupita chini ya kamba iliyopita juu ya kamba nyingine.

Matumizi:


- Kuunganisha kamba na vitu mbalimbali.
- Kupanda milima.

Clove hitch




20


Half Hitch




Clove Hitch Tied in the Open



Clove Hitch Tied Around an Object



NAMNA YA KUFUNGA TAI



24

